



DODOMA INSTITUTE OF DEVELOPMENT AND ENTREPRENEURSHIP STUDIES

Postal address: P. O. Box 2032, Dodoma

Website: www.dides.ac.tz Email: info@dides.ac.tz or didesvet@gmail.com

Mobile: +255 679 550 047, + 255 685 506 450, +255 769 550 047

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MAENDELEO YA JAMII KWA
NGAZI YA ASTASHAHADA (CHETI) NA STASHAHADA (DIPLOMA)- 2024/2025**

**A. MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI
VYETI NA VITAMBULISHO**

Tafadhali fika na cheti chako halisi cha kuzaliwa, cheti cha kidato cha nne au sita au cheti kutoka chuo kilichosajiliwa na NACTE.

JINSI YA KUFANYA MALIPO

Malipo yote yatalipwa kupitia kwenye control namba utakayopewa chuoni kwa na Ada ya Bweni ilipwe kwenye benki ya **CRDB; Account No. 0150681726000** kwa jina la *Dodoma Institute of Development and Entrepreneurship Studies* na uhifadhi bank slip zako vizuri.

Wanafunzi wote wanajitegemea kwa chakula; kwa kujipikia au kujinunulia kwenye migahawa na sehemu ya kupikia chakula ipo.

B. MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA MWANAFUNZI

i) MAHITAJI KWA AJILI YA MALAZI

- i. Shuka 2 (rangi yeyote)
- ii. Mto 1 wenye foronya
- iii. Chandarua.
- iv. Godoro jipya size ya 2.5 x 6 ft (futi mbili na nusu kwa sita) au 58,000/= kwa ajili ya kununua godoro kwa wale wanaotoka mbali.

ii) MAHITAJI KWA AJILI YA TAALUMA

- i. Gharama za masomo kwa mwaka kwa mwanafunzi wa Astashahada (**CHETI**) ni Tsh.1,310,000/= .Italipwa kwa **awamu nne**, kwa kuanzia yaani (awamu ya kwanza) mwanafunzi atalipa **Ada** na **Michango** Tsh **350,000/=** na Bweni Tsh. **100,000/=**. (Awamu ya pili) yaani katikati ya muhula wa kwanza mwanafunzi atalipa Tsh. **320,000/=**

- (Awamu ya tatu) yaani mwanzo mwa muhula wa pili mwanafunzi atalipa Tsh. **3200,000/=** na Bweni **Tsh 100,000/=** Awamu ya nne yaani katikati ya muhula wa pili atalipa Tsh **320,000/=** (kama ilivyoelekezwa kwenye fomu ya maombi.
- ii. Gharama za masomo kwa mwaka kwa mwanafunzi wa Stashahada (**DIPLOMA**) Tsh.**1,360,000/=**.Italipwa kwa **awamu nne**, kwa kuanzia yaani (awamu ya kwanza) mwanafunzi atalipa **Ada** na **Michango** Tsh **400,000/=** na Bweni Tsh. **100,000/=**.
(Awamu ya pili) yaani katikati ya muhula wa kwanza mwanafunzi atalipa Tsh. **320,000/=** (Awamu ya tatu) yaani mwanzo mwa muhula wa pili mwanafunzi atalipa Tsh.**320,000/=** na **Bweni Tsh 100,000/=** na awamu ya nne yaani katikati ya muhula wa pili atalipa **Tsh 320,000/=** kama ilivyoelekezwa kwenye fomu ya maombi.
- iii. Gharama ya 20,000/= ya kujiunga katika mfumo wa NACTVET (Nactvet Online Registration) hii itatumwa mapema kwenye namba ya chuo **0679 550 047** kwa jina la ***Dodoma Institute of Development and Entrepreneurship Studies - DIDES***
- iv. Tsh 10,000/= ya umoja wa wanafunzi ilipwe kwenye NMB Account Namba 51710032980 kwa jina la **DIDESSO**.
- v. Tsh 10,000/= ya Fomu ya maombi ilipwe kwenye NMB Account Namba **51710012075** kwa jina la ***Dodoma Institute of Development and Entrepreneurship Studies***
- vi. Gharama za Bima ya Afya NHIF 50,400/= ni lazima kama mwanafunzi hana Bima ya Afya.
- vii. Ream paper mbili A4.
- viii. Daftari kubwa (counter books) tano kwa nukuu zake za masomo.
- ix. Faili mbili kwa ajili ya kutunzia nyaraka zake- (Test, Assignment, Exams, Quiz etc)
- Utakapofika chuoni utafahamishwa juu ya sheria na taratibu za chuo. Aidha, utapewa mafunzo karibishi (orientation).

***Tunakukaribisha sana chuo cha DIDES na Makao makuu ya nchi DODOMA
Karibu jiji la Dodoma***

**Grace N John
MKUU WA CHUO**